# JARIDA la eGA

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

## Mamlaka ya Serikali Mtandao

Toleo la 10 | Oktoba - Desemba 2024

# RAIS DKT. SAMIA KUFUNGUA MKUTANO WA 5 WA SERIKALI MTANDAO

- Mkutano kufanyika Februari 2025, Jijini Arusha




**Kauli Mbiu**

*"Jitihada na Ubunifu wa Serikali Mtandao kwa utoaji wa Huduma za Umma kwa ufanisi"*

# Yaliyomo

Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu........iii

Salamu za Mwaka mpya kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi wa e-GA ........iv

Baraza la Mawaziri sasa Kidijitali........1

Rais Samia kufungua Mkutano wa 5 wa Serikali Mtandao Februari Jijini Arusha........2

Taasisi za Umma zatakiwa kutumia Mifumo rasmi ya Serikali Mtandao........3

Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali Mtandao unavyochochea matumizi sahihi na salama ya TEHAMA Serikalini........4

Mfumo wa NGAO kuimarisha zaidi Usalama wa Mifumo ya Serikali........6

Kamati ya Baraza la Wawakilishi yaipongeza e-GA ujenzi wa Mifumo........7

Matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho ni takwa la kisheria........8

Makosa 7 ambayo mtumishi anapaswa kuyaepuka katika matumizi ya serikali mtandao........9

e-GA yatoa Elimu kwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi........10

Kutoka katika kituo cha utafiti, ubunifu na uendelezaji wa serikali mtandao........11

Mfumo wa TSMS waboreshwa kuimarisha utoaji Mafunzo na Semina........11

Matukio katika picha ........12




## Kutoka Kwa Mkurugenzi Mkuu

Karibu katika toleo la kumi la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Katika toleo hili la 10 utasoma na kujifunza kuhusiana na kazi na huduma mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka kama vile ujenzi wa mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya Taasisi husika, utoaji wa huduma za ushauri na msaada wa kiufundi, uboreshaji wa njia za utoaji wa huduma za Serikali Mtandao, utengenezaji na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini, inayosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini na utoaji wa huduma bora kwa umma.

Hali kadhalika, katika Jarida hili utafahamu juhudi na shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka katika utekelezaji wa dhana ya Serikali Mtandao.

Toleo hili ni muendelezo wa matoleo mengine yaliyopita yanayokuhabarisha kuhusu jitahada za e-GA katika kukuza na kuchochea matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Serikalini, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Nitumie fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kuifahamu vizuri e-GA na shughuli mbalimbali inazozitekeleza.

Nakutakia usomaji mwema.

Mhandisi Benedict B. Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**



# Salamu za Mwaka Mpya

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali(e-GA) napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuuona Mwaka Mpya wa 2025,na niwatakie nyote Heri ya Mwaka Mpya 2025.

Aidha, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuiwezesha e-GA kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Katika mwaka uliopita (2024), e-GA imeweza kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa taasisi za umma.

Utekelezaji wa majukumu haya, unatokana na mchango mkubwa wa Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Ofisi ya Rais, kwa kutenga bajeti na kuisimamia vema e-GA, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Pamoja na mafanikio haya, Mwaka huu mpya wa 2025 unaleta fursa mpya, changamoto, na matumaini mapya kwa Mamlaka, kuongeza jitihada na kuboresha mikakati ya kuziwezesha Taasisi za Umma kutumia TEHAMA katika utendaji kazi wake, ili kuongeza ufanisi pamoja na kuboresha utoaji wa huduma bora kwa umma.

Ili tufikie malengo ya kuwa na Serikali ya kiidijiti imara na yenye tija, jitihada za pamoja zinahitajika kwa wadau wote wa Serikali Mtandao, kwa kuhakikisha wanazingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika ujenzi na usimamizi wa miradi na mifumo ya TEHAMA Serikalini.

Nitumie nafasi hii kutoa wito kwa Wizara, Wakala, Idara za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekta Binafsi na wadau wote wa Serikali Mtandao kushirikiana kikamilifu na Mamlaka, katika kufanikisha malengo yetu ya kuleta mapinduzi ya kidijiti Serikalini na kufanya huduma za Serikali kuwa bora zaidi kwa mwaka mpya wa 2025.

Tunapenda kuwashukuru kwa ushirikiano wenu wa karibu mwaka uliopita na tunatarajia kuendelea kushirikiana kwa karibu zaidi kwa mwaka 2025.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha wote katika Mkutano wa Tano (5) wa Mwaka wa Serikali Mtandao, unaotarajiwa kufanyika tarehe 11 – 13 Februari 2025, katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

Katika Mkutano huu, tutakuwa na fursa ya kujadili kwa pamoja na kuweka mikakati ya kuimarisha na kukuza jitihada za Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma, na kuimarisha ushirikiano wetu ili kuhakikisha utoaji wa huduma serikalini kidijitali unaimarika zaidi.

Heri ya Mwaka Mpya 2025! Tushirikiane kwa pamoja katika safari hii ya kuijenga Serikali yaKidijiti.

**Dkt. Mussa Kissaka**
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi

# BARAZA LA MAWAZIRI SASA KIDIJITALI - MAJALIWA



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akizungumza na Mawaziri na Manaibu Mawaziri wakati akifungua Mafunzo ya Mfumo wa e-CABINET tarehe 11 Novemba 2024, jijini Dodoma.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), amesema kuwa matumizi ya Mfumo wa Kielektroni wa Baraza la Mawaziri (e-Cabinet), yanalenga kurahisisha utendaji kazi wa baraza hilo sambamba na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mhe. Majaliwa aliyasema hayo Novemba 11, 2024 wakati akifunga Mkutano wa Kazi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri, kuhusu matumizi ya mfumo wa e-CABINET, uliofanyika katika ukumbi wa Hazina jijini Dodoma

Amebainisha kuwa, mfumo huo utasaidia kupunguza matumizi ya karatasi katika vikao vya Serikali, hususan Baraza la Mawaziri na hivyo kuokoa fedha za Serikali zilizokuwa zikitumika katika ununuzi wa karatasi.

"Mfumo huu utaturahisishia utendaji kazi na kuweza kuwahudumia wananchi kwa wakati na kutatua changamoto mbalimbali zikiwemo kuchelewa kwa taarifa na hatari ya upotevu wa taarifa muhimu", amesema Mhe. Majaliwa.

Ameongeza kuwa, ujenzi wa mfumo huo unatokana na jitihada za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuleta mageuzi ya kidijitali Serikalini kupitia Mamlaka ya Serikali Mtadao (e-GA) .

Amesema kuwa, kutokana na jitihada na nia thabiti ya Mhe. Rais katika matumizi ya teknolojia Serikalini, Tanzania imeweza kupiga hatua kubwa katika matumizi ya teknolojia na kuongoza katika ukanda wa Afrika Mashariki.

**"Matokeo ya utafiti wa mwaka 2022 uliofanywa na Benki ya Dunìa kuhusu ulinganifu baina ya nchi katika muktadha wa Ukomavu wa Matumizi ya Teknolojia Serikalini (Government Technical Maturity Index), nchi yetu ilishika nafasi ya tatu (3) ikilinganishwa na nchi nyingine Barani Afrika na hii ni kutokana na jitihada za Mhe. Rais katika uwekezaji kwenye matumizi ya teknolojia"**

**Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa**
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ameongeza kuwa, matumizi ya mfumo huo ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuhakikisha kwamba, Mawaziri na watumishi wa umma wanakuwa na ujuzi wa kisasa wa uendeshaji wa shughuli za Serikali na utumishi kwa ujumla kupitia TEHAMA.
Aidha, amefafanua kuwa uanzishwaji wa mfumo huo wa e-Cabinet, ni utekelezaji wa Ibara za 102 na 103 za Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 zinazoelekeza Serikali kuhakikisha kuwa sayansi, teknolojia na ubunifu vinatumika kikamilifu katika kuendesha sekta za kukuza uchumi kwa lengo la kufikia uchumi wa hadhi ya kipato cha kati ambao ni shindani, jumuishi na unaoongozwa na viwanda.

Kwa Upande wake, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko (Mb) amewapongeza wataalam kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kufanikisha mafunzo hayo, na kuwataka kuendelea na jitihada mbalimbali za ujenzi wa Serikali ya Kidijiti.

Naye, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (Mb), amesema kuwa mafunzo hayo ni mwendelezo wa mpango wa Serikali kwenda kwenye matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa Baraza La Mawaziri (e-CABINET).

Amebainisha kuwa, mchakato wa ujenzi wa mfumo huo ulikuwa ni wa muda mrefu kupitia wataalam wa e-GA, na kuahidi kuendelea kuisimamia vema Mamlaka hiyo ili kuhakikisha matumizi ya TEHAMA Serikalini yanaimarika katika sekta zote.




# RAIS DKT. SAMIA KUFUNGUA MKUTANO WA 5 WA SERIKALI MTANDAO JIJINI ARUSHA

Takriban wadau 1000 wa serikali mtandao wanatarajiwa kukutana kwa siku tatu, kuanzia Februari 11 hadi 13, 2025 Jijini Arusha, ili kujadiliana kuhusu hali ya utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini, kuainisha changamoto, sambamba na kuweka mikakati ya pamoja ya kukabiliana na changamoto hizo.

Wadau hao kutoka katika taasisi na mashirika mbalimbali ya umma, wanatarajiwa kukutana katika Mkutano wa (5) wa mwaka wa Serikali Mtandao, utakaofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC).

Akizungumza kuhusu mkutano huo, Meneja Mawasiliano wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Subira Kaswaga amesema, mkutano huo utafunguliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuoneshwa mubashara katika vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii.

Ameongeza kuwa, mkutano huo utawakutanisha viongozi na watumishi mbalimbali wa sekta ya umma wakiwemo Makatibu Wakuu, Maafisa Masuuli, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na vitengo vya TEHAMA, Maafisa TEHAMA pamoja na Maafisa wa kada nyingine.

"Lengo la mkutano huo ni kuwakutanisha wadau wa Serikali Mtandao kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, ili waweze kujadili kwa pamoja jitihada mbalimbali za utekelezaji wa Serikali Mtandao, na kuweka mikakati itakayosaidia kukuza jitihada hizo", amefafanua Bi. Subira.

Ameongeza kuwa, mkutano huo unatarajiwa kuongeza uelewa kwa washiriki kuhusu serikali mtandao, teknolojia mpya zinazoibukia sambamba na namna zinavyoweza kutumika katika kuimarisha utendaji kazi serikalini na kurahisisha utoaji wa huduma bora kwa umma.

"Mkutano huo utaongozwa na kauli mbiu isemayo ***"Jitihada na Ubunifu wa Serikali Mtandao kwa utoaji wa huduma za umma kwa Ufanisi"*** ikiwa na lengo la kuchochea ubunifu na utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma, ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa umma", amesema Bi. Subira.

Amefafanua kuwa, katika mkutano huo, e-GA itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio 12 yaliyoafikiwa katika Mkutano wa nne (4) wa Serikali Mtandao uliofanyika Februari 2024.

"Katika mkutano uliopita, wadau waliweka maazimio 12 yaliyolenga kuboresha utendaji kazi na utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, hivyo mwaka huu tutawasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo kwa washiriki wote" ameeleza Bi. Subira.

Aidha, Bi.Subira ametoa rai kwa wadau wote wa Serikali Mtandao kutoka sekta ya umma kujitokeza kwa wingi na kushiriki kikamilifu katika mkutano huo, kwa kujisajili kupitia mfumo wa mafunzo na semina (TSMS) unaopatikana kwa anuani ya www.tsms.gov.go.tz.




Wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao wakiwa katika kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao kilichofanyika jijini Arusha Februari 2024

# TAASISI ZA UMMA ZATAKIWA KUTUMIA MIFUMO RASMI YA SERIKALI MTANDAO



Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar Mhe.Machano Othman Said akizungumza wakati wa Ziara ya kamati hiyo katika Ofisi za e-GA Jijini Dodoma

Taasisi za umma zimetakiwa kutumia mifumo rasmi ya serikali iliyoidhinishwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ili kulinda usalama wa taarifa za serikali sambamba na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi hizo.

Wito huo umetolewa na Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wakati ilipofanya ziara ya kikazi ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mtumba jijini Dodoma Oktoba 25, 2024.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe.Machano Othman Said, alisema kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imepewa dhamana ya kuidhinisha mifumo ya TEHAMA Serikalini hivyo ni wajibu wa taasisi za umma kuhakikisha zinazingatia utaratibu na kutumia mifumo iliyoidhinishwa na e-GA.

Alibainisha kuwa, lengo la Serikali kuanzisha e-GA ni kudhibiti upotevu wa fedha za umma katika miradi ya TEHAMA sambamba na kuhakikisha udhibiti na usalama wa taarifa za serikali kupitia mifumo ya TEHAMA.

”Tumeelezwa hapa ipo mifumo ambayo imetengenezwa na e-GA inayotumika serikalini lakini pia ipo mifumo mingine katika taasisi mbalimbali za umma iliyotengenezwa na wakandarasi, jambo muhimu ni taasisi hizo kuhakikisha mifumo yao imeidhinishwa na e-GA ili kuimarisha udhibiti na usalama wa taarifa za serikali”, alisema Mhe. Machano.

Aliongeza kuwa, ili mifumo ipate idhini ya e-GA ni lazima uanzishwaji na uendeshaji wa mifumo hiyo uzingatie Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kuanzia hatua za awali za uanzishwaji wake.

Katika hatua nyingine, Mhe.Machano alipongeza e-GA kwa kuimarisha ushirikiano na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), katika jitihada mbalimbali za ujenzi wa Serikali Mtandao.

”Kutokana na ushirikiano mzuri uliopo kati ya Mamlaka hizi mbili tunashuhudia mafanikio ya ushirikiano huu hasa katika ujenzi wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA ambayo inatumika bara na visiwani na hii ndio maana halisi ya kuwa na maendeleo ya pamoja ” alifafanua Mhe. Machano.

Aliongeza kuwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Mapinduzi ya Zanzibar imeonesha dhamira ya dhati katika kuboresha huduma za serikali kidijiti, kwa kutenga fedha za miradi mbalimbali ya TEHAMA nchini.

“Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan na Dkt.Hussein Mwinyi, wamekuwa vinara katika kuleta mapinduzi ya kidijiti na kuonesha umuhimu wa TEHAMA katika utendaji, hivyo tusisitize Taasisi zote kutumia mifumo ya TEHAMA inayotengenezwa na Mamlaka zetu za Serikali Mtandao katika utendaji kazi wao wa kila siku” alisisitiza Mh.Machano.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba, aliahidi kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar ili kuhakikisha matumizi ya TEHAMA serikalini yanazidi kuimarika ili kuimarisha utawala bora, kudhibiti mapato ya serikali na kulinda usalama wa nchi katika zama hizi za sayansi na teknolojia.

Kamati hiyo iliambatana na Mhe. Ali Suleiman Ameir - Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu Zanzibar, Ndg. Saleh Juma Mussa - Katibu Mkuu - Afisi ya Rais, Ikulu Zanzibar pamoja na Watendaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ).



**“Tumefurahishwa sana na ziara hii, kwani ni ishara njema kwetu kuona mnatuthamini na kutambua umuhimu wa kazi tunazozifanya, lakini pia tumeona ni jinsi gani ushirikiano wetu na e-GAZ unavyoleta matokeo chanya, niwaombe muendelee kuwa mabalozi wazuri wa huduma za Serikali Mtandao zinazosanisifiwa na Mamlaka zetu”**

Mhandisi Benedict Ndomba.
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

# USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA SERIKALI MTANDAO UNAVYOCHOCHEA MATUMIZI SAHIHI NA SALAMA YA TEHAMA SERIKALINI



Ufanisi wa Serikali Mtandao hutegemea usimamizi mzuri wa rasilimali, ushirikiano wa wadau, na utekelezaji wa mikakati madhubuti ili kuiwezesha Serikali kutoa huduma bora, kupunguza urasimu, na kuongeza uwazi, na hatimaye kuboresha maisha ya wananchi.

Katika kuhakikisha usimamizi thabiti wa Serikali Mtandao nchini, Kifungu cha 15 cha Sheria ya Serikali Mtandao Namba 10 Sura ya 273 ya Mwaka 2019 (Sheria), kinaelekeza juu ya uanzishwaji wa muundo na michakato ya Serikali-mtandao katika utumishi wa umma, ambapo kamati mbalimbali za Uongozi za Serikali Mtandao katika taasisi za umma zimeanzishwa.

Kamati hizo ni Kamati ya Kitaifa ya Uongozi ya Serikali-mtandao, Kamati ya Ufundi ya Serikali-mtandao na Kamati ya Kitaasisi ya Uongozi ya Serikali-mtandao.

Lengo kuu la kuanzisha kamati hizi, ni kutoa miongozo katika kusimamia na kudhibiti utekelezaji wa matumizi sahihi ya TEHAMA katika taasisi zote za umma zikiwemo Wizara, Halmashauri, Mashirika ya Umma na Idara za Serikali zinazojitegemea.

Kifungu cha 16 (1) cha Sheria kinaanzisha Kamati ya Kitaifa ya Uongozi ya Serikali Mtandao (National e-Government Steering Committee), kwa ajili ya kusimamia masuala ya kitaifa ya Serikali Mtandao.

Pia kifungu cha 16(2) cha Sheria, kinatoa muundo wa kamati hiyo ambayo itaundwa na Katibu Mkuu Kiongozi ambaye ndiye atakua Mwenyekiti wa kamati na Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na kusimamia Serikali Mtandao ndiye atakua Katibu.

Wajumbe wengine wa kamati hii ni Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na TEHAMA nchini (Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari), Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na fedha (Wizara ya Fedha), Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Aidha, Wizara yenye dhamana na Serikali Mtandao, itatumika kama sekretarieti ya Kamati ya Kitaifa ya Uongozi ya Serikali Mtandao.

Meneja wa Kitengo cha Huduma za Sheria e-GA, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Raphael Rutaihwa, amebainisha kwamba kamati hii imekasimiwa majukumu matano (5) makubwa ikiwemo, kutoa miongozo ya kimkakati na kisera inayohitajika kuendesha mabadiliko ya utoaji na utawala wa huduma za umma katika zama za kidijiti.

Ameongeza kuwa, kamati hii pia imepewa jukumu la kuidhinisha sera mtambuka za TEHAMA, mikakati, mpango mkuu na miongozo katika Serikali pamoja na kushauri juu ya miradi na mipango muhimu ya TEHAMA, ili kuhakikisha matumizi shirikishi na ya gharama nafuu ya TEHAMA katika Serikali.



**SACP. Raphael Rutaihwa**

**“Vilevile, kamati hii imepewa jukumu la kumshauri Waziri mwenye dhamana juu ya masuala yote yanayohusu Serikali Mtandao, na kutekeleza majukumu mengine kama ambavyo Waziri anaweza kuelekeza”.**

**SACP. Raphael Rutaihwa**

Aidha, Kifungu cha 17(1) cha Sheria kimemtaka Waziri mwenye dhamana ya Serikali Mtandao, kuunda Kamati ya Ufundi ya Serikali Mtandao (e-Government Technical Committee), kwa ajili ya kutoa mwongozo wa kiufundi kwa taasisi za umma juu ya utekelezaji wa mipango ya TEHAMA.

Kwa mujibu wa kifungu cha 17(2) cha Sheria, Wajumbe wa Kamati hii watateuliwa kutoka miongoni mwa Wakuu wa Idara na Vitengo vya TEHAMA katika Wizara, na Wakurugenzi wa Ufundi wa TEHAMA wa taasisi za umma ambazo zimetajwa kisheria.

Mwenyekiti wa Kamati hii atateuliwa na Waziri na Katibu atateuliwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kama ambavyo kifungu cha 17(3) cha Sheria kinaelekeza.

Aidha, Kamati hii ya Ufundi chini ya kifungu cha 17(4) cha Sheria ina jukumu la kupitia na kupendekeza juu ya sera ya Serikali Mtandao, kwa ajili ya matumizi ya taasisi zote za umma.

Pamoja na majukumu mengine ya msingi kama vile kuidhinisha viwango vya Serikali Mtandao, kupitia na kupendekeza juu ya miradi na mipango muhimu ya kitaifa ya Serikali Mtandao, pamoja na kuishauri Kamati ya Kitaifa ya Uongozi ya Serikali-mtandao juu ya masuala yote yanayohusiana na Serikali-mtandao.

Aidha, kamati ya Ufundi ya Serikali Mtandao, katika utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii, itawajibika na kuripoti kwa Kamati ya Kitaifa ya Uongozi ya Serikali-mtandao, kwa kuandaa taarifa ya shughuli zake kila robo mwaka na kuiwasilisha kwa Kamati ya Uongozi ya Serikali Mtandao, kama ambavyo kifungu cha 17(5) na (6) cha sheria ya Serikali Mtandao kimeelekeza.

Kamati hii pia, kwa ajili ya utendaji bora wa majukumu yake chini ya kifungu kidogo cha (4) imepewa nguvu ya kuunda kamati ndogo kwa idadi itakayofaa, ili kutekeleza majukumu ya kiufundi kama inavyoweza kuamua, lengo ni kuhakikisha kamati hii inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Kamati nyingine ni ile inayopaswa kuundwa katika ngazi ya taasisi, Kifungu cha 18 (1) cha Sheria kinamtaka kila Afisa Masuuli wa taasisi ya umma kuunda Kamati ya Kitaasisi ya Uongozi ya TEHAMA (Institutional ICT Steering Committee) ambayo itasimamia utekelezaji wa muongozo wa TEHAMA katika taasisi husika.

Lengo ni kuhakikisha miradi na mifumo yote ya TEHAMA inazingatia Sheria ya Serikali Mtandao na kuleta tija kwa taasisi husika kulingana na thamani halisi ya uwekezaji iliyowekwa.

Sambamba na hilo, Kifungu cha 18(2) cha Sheria, kinaelekeza uundaji wa Kamati ya Kitaasisi ya Uongozi ya TEHAMA ambayo itaundwa na wajumbe wasiopungua sita (6) na wasiozidi saba (7) kama ifuatavyo; Afisa Masuuli wa taasisi husika atakuwa Mwenyekiti na Mkuu wa Idara/Kitengo cha TEHAMA ambaye atakuwa katibu wa Kamati.

Wajumbe wengine ni Mkuu wa Mipango; Mkuu wa Ununuzi; Mkaguzi Mkuu wa Ndani; Mhasibu Mkuu; na angalau Mkuu mmoja wa Kitengo au Idara inayohusika na shughuli kuu ya biashara inayozalishwa katika taasisi (head of key business unit).

Kamati ya Kitaasisi ya Uongozi ya TEHAMA itatekeleza majukumu makuu saba (7) kama yalivyoainishwa chini ya kifungu cha 18(3) cha Sheria ikiwemo; kukagua na kupitisha sera na mikakati ya TEHAMA ya taasisi; kukagua na kutoa ushauri juu ya uwekezaji wa TEHAMA na vipaumbele vyake.

Majukumu mengine ni kuhakikisha ufuatiliaji na tathmini endelevu ya miradi ya TEHAMA ya kitaasisi; kukagua na kupitisha mipango ya maafa ya kitaasisi na hakikisha utekelezaji wake unafanikiwa.

Aidha, kifungu cha 18(7) cha Sheria kimeelekeza kamati hii kuwajibika kuandaa na kuwasilisha ripoti ya robo mwaka kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ikieleza maendeleo ya jitahada za Serikali Mtandao katika taasisi husika; na kutekeleza majukumu mengine kama inavyoweza kuelekezwa na Afisa masuuli au Mamlaka.

Hadi sasa uwepo wa Kamati ya Uongozi za Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma zikiwemo halmashauri, zimeongeza ufanisi katika matumizi ya serikali mtandao nchini na kuhakikisha miongozo na viwango vya Serikali Mtandao vinatekelezwa ipasavyo.

Meneja wa Usimamizi wa Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao wa e-GA Bi. Sultana Seiff, amebainisha kwamba kamati hizo zimekuwa kiungo muhimu katika ukuzaji wa jitihada za Serikali Mtandao katika taasisi za umma na kurahisisha huduma za serikali kwa wananchi.



**“Kamati hizi zina mchango mkubwa katika kukuza na kuimarisha matumizi ya TEHAMA ndani ya taasisi, ikiwemo utekelezaji wa miradi mbalimbali ya TEHAMA ambayo inachangia katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi ndani ya taasisi na kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi,”**

**Bi. Sultana Seiff**


Ameongeza kuwa, kamati hizi pia zimekuwa kiungo muhimu katika utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika matumizi ya TEHAMA ndani ya taasisi husika.

Kwa upande wake SACP Rutaihwa ametoa rai kwa taasisi zote za umma zikiwemo halmashauri kuanzisha kamati za Uongozi wa TEHAMA ndani ya Taasisi zao. ili kukidhi takwa la kifungu cha 18 cha Sheria ya Serikali Mtandao.

Usimamizi na uendeshaji wa serikali mtandao unatoa fursa kubwa ya kuboresha utendaji wa serikali, kuongeza uwazi, na kuboresha huduma kwa wananchi. Kwa kutumia TEHAMA, serikali ina uwezo wa kufikia wananchi wengi kwa urahisi zaidi, kutoa huduma kwa ufanisi, na kupunguza urasimu.

Ili kufanikisha malengo haya, ni muhimu viongozi wa taasisi za umma kuhakikisha wanaunda kamati za uongozi wa TEHAMA katika taasisi zao sambamba na kamati zote tatu kuhakikisha zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi kama yalivyoainishwa katika sheria.

# MFUMO WA NGAO KUIMARISHA ZAIDI USALAMA WA MIFUMO YA TEHAMA SERIKALINI




Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imetengeneza Mfumo wa Usalama wa Kidijiti wa Uthibitishaji wa vipengele vingi ujulikanao kama NGAO, utakaotumika kuhakikisha usalama wa ziada wa taarifa muhimu kwa watumiaji wa mifumo ya Serikali.

Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Sylvani Shayo amesema, mfumo wa NGAO unalenga kuhakikisha watumiaji wanaweza kufikia mifumo ya Serikali kwa njia salama zaidi, kupunguza hatari za udukuzi na matumizi mabaya ya taarifa za serikali.

Bw. Shayo ameeleza kuwa, mfumo wa NGAO unatumia programu ya 'NGAO Authenticator' inayotengeneza nenosiri (nywila) ya mara moja (One-Time Password - OTP), kwa kila uthibitisho wa mtumiaji ambayo itasaidia kuimarisha usalama wa watumiaji kwa kutoa tabaka lingine la ulinzi zaidi ya baruapepe ya mtumiaji na nenosiri.

" Kila mtumiaji wa mifumo ya TEHAMA, hupaswa kuweka baruapepe anayotumia na nenosiri kila anapotaka kuingia kwenye mfumo, hii ni hatua ya awali na ya kawaida lakini kupitia mfumo huu wa NGAO kutakuwa na hatua ya pili baada ya kuingia kwenye mfumo, mtumiaji atahitaji kuthibitisha utambulisho wake kwa kutumia njia nyingine, kama vile kupitia ujumbe mfupi (SMS) kwenye simu yake ya kiganjani", amesema Shayo.

Amebainisha kuwa, mfumo wa NGAO utasaidia kupunguza hatari za udukuzi kupitia njia za kawaida za nenosiri kwa kuhitaji uthibitisho wa ziada pamoja na kujenga uaminifu wa watumiaji kwakuwa taarifa zao zinahifadhiwa kwa usalama na zinaweza kufikiwa tu na watu waliothibitishwa.

**"Umuhimu wa NGAO ni mkubwa sana katika kulinda taarifa nyeti za Serikali na kutoa mazingira salama kwa watumiaji wa mifumo ya Serikali na hivyo kumuwezesha anayehusika tu na taarifa hizo kuweza kuzifikia"**

**Bw. Sylvani Shayo**
**Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA e-GA**

Ameongeza kuwa, mfumo huo unawawezesha watumiaji wa mifumo ya Serikali kupokea taarifa kwenye simu zao za kiganjani kila wanapojaribu kuingia kwenye mfumo, na kupewa nafasi ya kukubali au kukataa ombi la kuingia, lakini pia kupokea taarifa za uthibitisho kwenye laini za simu bila hitaji la mtumiaji kuwa na mtandao wa intaneti.

Kwa sasa, mfumo wa NGAO unatumiwa kwa majaribio na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) pekee katika Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office) na Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS), huku malengo yakiwa ni kuongeza matumizi ya mfumo huo katika mifumo mingine ya Serikali ili kuhakikisha usalama wa taarifa na kuimarisha ufanisi katika shughuli za Serikali Kidijitali.



**Bw. Sylvani Shayo**
Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

# KAMATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI YAIPONGEZA e-GA KUTUMIA WATAALAMU WA NDANI KATIKA UJENZI NA USANIFU MIFUMO YA TEHAMA SERIKALINI.



Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba akiwasilisha taarifa ya Utendaji wa e-GA kwa kamati ya Baraza la Wawakilishi ya kuchunguza na kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (PAC) .

KAMATI ya Baraza la Wawakilishi ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (PAC), imeiopongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kutumia wataalamu wa ndani katika ujenzi na usanifu wa mifumo ya TEHAMA Serikalini.

Pongezi hizo zimetolewa Desema 16, 2024 na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mh. Juma Ali Khatib, baada ya kupokea wasilisho kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba, wakati wa ziara fupi ya kamati hiyo katika ofisi za e-GA jijini Dodoma.

Alibainisha kuwa, uamuzi wa kutumia wataalamu wa ndani ni hatua muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya e-GA katika kusimamia, kuratibu na kukuza jitihada za Serikali Mtandao kwa kutumia vema rasilimali zilizopo na kudhibiti usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA serikalini.

“Tunawapongeza e-GA kwa kutumia vijana wa kitanzania kutengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA inayotumika serikalini, lakini pia kwa kuendesha Kituo cha Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao, ili kukuza na kuibua vipaji vya vijana wazawa”, alisema Mh. Khatib.

Sanjari na hilo, Mh.Katib alipongeza utendaji kazi wa e-GA na eGAZ na kuwasihi watumishi wa mamlaka hizo kuendelea na nidhamu, uadilifu na juhudi katika kutekeleza majukumu yao.

**”Tupo tayari kushirikiana na wenzetu (e-GAZ) katika kuhakikisha maono ya Serikali ya awamu ya sita (6) ya kuwa na serikali ya kidijiti yanatimia katika kutoa huduma bora kwa wananchi kwa wakati, mahali popote na kwa gharama nafuu”.**

Mhandisi Benedict Ndomba.

**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

“Tangu kuanzishwa kwa e-GA na eGAZ hatujawahi kusikia tukio lolote la kinidhamu lenye kuhatarisha usalama wa mifumo hii ya serikali,hivyo niwapongeze na kuwasihi muendeleze nidhamu na uadilifu mlionao na kuwa mfano mzuri kwa umma”, alieleza.

Aliongeza kuwa, Serikali ya Tanzania chini ya Rais Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Mapinduzi chini ya Dkt.Hussein Mwinyi, imedhamiria kuleta mageuzi ya TEHAMA hivyo, ameitaka e-GA kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), ili kutimiza malengo hayo ya Serikali.

Mkurugenzi wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba, aliishukuru kamati hiyo kufanya ziara hiyo na kuahidi kuyafanyia kazi yale yote ambayo kamati hiyo imeyaelekeza ikiwemo kuhimarisha ushirikiano kati ya e-GA na e-GAZ.

# MATUMIZI YA MFUMO WA e-MREJESHO NI TAKWA LA KISHERIA: UTUMISHI



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Xavier Daudi .

Taasisi zote za Umma zatakiwa kujiunga na kuutumia mfumo wa e-Mrejesho ili kuweza kutatua changamto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Hayo yamesemwa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Xavier Daudi wakati akifunga kikao kazi cha mafunzo ya mfumo wa e-Mrejesho yaliyofanyika katika Ukumbi wa Makumbusho ya Taifa Oktoba4, 2024.

"Kabla ya mwezi huu Oktoba kuisha taasisi zote za Umma ambazo bado hazijaanza kutumia mfumo wa e-Mrejesho zianze kuutumia mfumo huu na kuhakikisha kero zote zinazowasilishwa ndani ya mfumo zinafanyiwa kazi"amesema Daudi.

Naibu Katibu Mkuu huyo amesema kuwa matumizi ya mfumo wa e-Mrejesho ni takwa la kisheria na sio maamuzi ya taasisi kutumia au kutotumia mfumo huo kwani kwakutokushughulikia kero zinazowasilishwa nikuwanyima wananchi haki za msingi.

Aidha, Naibu Katibu Mkuu huyo amewaagiza viongozi wa taasisi zote za Umma kuhakikisha wanaimarisha dawati la mrejesho kwakuweka watumishi wenye weledi na wanaoweza kutunza siri.

Vilevile amewataka viongozi wa Taasisi za Umma kuhakikisha maofisa mrejesho wote wanapatiwa mafunzo ya mara kwa mara ili kuwajengea uwezo wa kutatua changamoto mbalimbali zinazo wasilishwa kwenye dawati hilo la mrejesho.

Akishukuru kwa niaba ya washiriki wote Mwenyekiti wa kikao kazi hicho Bw. Fadhili Sultani amesema kuwa anaishukuru Ofisi ya Rais - Utumishi pamoja na e-GA kwa kuandaa mafunzo hayo.

Aidha, Mwenyekiti huyo ameomba hoja zote zilizowasilishwa kwa ajili ya kufanyiwa maboresho zifanyiwe kazi mapema ili wapate fursa ya kuupitia mfumo huo kabla haujaanza kutumika rasmi.


Bw.Sultani pia ameomba watumishi wa taasisi nyingine ambao hawajapata fursa ya kuhudhuria mafunzo hayo wapatiwe nafasi ya kupitishwa kwenye mfumo huo ili waweze kutoa maoni yao.

Naye Mkurugenzi wa Usimamizi wa Udhibiti na Usalama wa Mifumo ya TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Silyvan Shayo amesema e-GA ipo tayari kushirikiana na Ofisi ya Rais - Utumishi na kuhakikisha maboresho yote yanafanyiwa kazi kwa wakati kama wadau walivyoomba.

Kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi Bi . Leila Mavika, Mkurugenzi wa Maadili kutoka Ofisi ya Rais Menejimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora amesema kuwa kundi hili la kwanza la maafisa waliopatiwa mafunzo hayo ni Maafisa Mrejesho na TEHAMA wapatao 105 ambao taasisi zao zinafanya vizuri katika kutumia mfumo wa e-Mrejesho.

**Mfumo wa e-Mrejesho unafanya kazi kwa ufanisi na unapatikana wakati wote kupitia simu za mkononi**

- *152*00#
- Aplikesheni tumizi ya e-Mrejesho
- Tovuti: www.emrejesho.gov.go.tz



# FAHAMU MAKOSA SABA (7) AMBAYO MTUMISHI WA UMMA ANAPASWA KUYAEPUKA KATIKA MATUMIZI YA SERIKALI MTANDAO

Serikali Mtandao ni matumizi ya TEHAMA katika utendaji wa kazi Serikalini na utoaji wa huduma kwa wananchi, dhamira kuu ya Serikali Mtandao ni kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kwa urahisi na haraka zaidi mahali walipo.



Ili kuhakikisha dhamira ya ujenzi sahihi wa Serikali Mtandao inafikiwa, Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10, Sura Na. 273 ya Mwaka 2019, inatoa muongozo wa namna bora ya matumizi sahihi na salama ya ujenzi wa Serikali Mtandao pamoja na kuainisha makosa ya matumizi ya Serikali Mtandao na adhabu zake kwa watumishi wa umma.

Makosa haya yameainishwa kwa watumishi wa umma kwakuwa, wao haswa ndio watumiaji na watekelezaji wakuu wa Serikali Mtandao ambao hutekeleza majukumu yao kupitia mifumo mbalimbali ya TEHAMA na miundombinu yake ili kuwezesha upatikanaji wa huduma kwa wananchi kidijitali.

Ikiwa watumishi wa umma watakosa weledi na uzalendo, dhamira ya Serikali Mtandao haiwezi kufikiwa na ndipo Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10, Sura Na. 273 ya Mwaka 2019 kupitia Kifungu cha 57(1), ikabainisha makosa saba (07) ambayo mtumishi wa umma anapaswa kuyaepuka ili kuwa na Serikali Mtandao yenye tija.

Kosa la kwanza (a) kufichua 'disclosure' kushirikisha taarifa za kiofisi au kumbukumbu yoyote ya kielektroniki iliyopatikana wakati wa ajira kwa watu wasiohusika. Mtumishi wa umma hapaswi kufichua au kushirikisha taarifa kutoka ofisi ya umma kwa mtu au makundi sogozi kupitia mitandao ya kijamii kama vile 'WhatsApp', 'Instagram', 'Facebook' n.k ufichuaji na ushirikishaji wa taarifa za Serikali unapaswa kufanywa kwa kufuata utaratibu wa kiofisi ulioainishwa tu na si vinginevyo.

Kosa la pili (b) ni kupakua 'download' mafaili yasiyoidhinishwa kwa kutumia vifaa vya kieletroniki vya ofisi kama vile Kompyuta, flash, intaneti n.k. Mfano wa mafaili haya ni filamu au nyimbo za muziki. vifaa vya ofisi vinapaswa kutumika kwa shughuli za kiofisi tu.

Kosa la tatu (c) ni kusambaza 'disseminate' au kutuma 'transmit' taarifa rasmi au data za serikali kupitia njia zisizoidhinishwa, kwa mujibu wa Mwongozo wa Matumizi Bora, Sahihi na Salama ya Vifaa na Mifumo ya TEHAMA Serikalini wa mwaka 2022 (kipengele na 3.3.8), njia iliyoidhinishwa ya usambazaji wa taarifa za Serikali, ni kupiti Mfumo wa Barua pepe za Serikali (GMS), hivyo kusambaza au kutuma taarifa za Serikali kupitia baruapepe nyingine ni kosa kisheria.

Kosa la nne (d) ni kuzifikia au kupata taarifa au program za Serikali kupitia vifaa vya TEHAMA vya serikali bila idhini. Mtumishi wa umma anayetakiwa kuzifikia taarifa au vifaa hivyo ni yule tu aliyepewa idhini kwa mujibu wa sheria na taratibu za kiofisi. Si kila mtumishi wa umma anapaswa kuzifikia taarifa zote za Serikali bali ni wale tu wanaoruhusiwa na walioidhinishwa kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Kosa la tano (e) ni kosa la kuondoa, kuharibu au kubadili data, kumbukumbu za kielektroniki, mifumo au vifaa vya kielektroniki isivyo halali. Mfano wa kosa hili ni kuharibu kwa nia ovu kompyuta ya ofisi au taarifa muhimu za Serikali, kwa lengo la kupoteza Ushahidi au kwa maslahi binafsi kwa kushirikiana na watu wenye nia ovu.

Kosa la sita (f) ni kushindwa kufuata kwa kujua au kwa uzembe; miongozo ya kiufundi na viwango vilivyowekwa kuhusu masuala ya usalama. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imeandaa Miongozo na Viwango vya Serikali Mtandao ambayo inapaswa kufuatwa na taasisi zote za umma katika masuala ya usalama wa TEHAMA. hivyo watumishi wa umma wanapaswa kuizingatia miongozo hiyo.

Kosa la saba (g) ni kutofuata taratibu na miongozo iliyowekwa katika uanzishwaji wa miradi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, miradi yote ya TEHAMA ni lazima ifuate utaratibu kama ilivyoelezewa katika kifungu cha 24 cha sheria hii, na ukiukwaji wa utekelezaji ni kosa kwa mujibu wa sheria hii.

Sheria imeweka wazi adhabu za makosa haya kwa kosa namba 1,3,4 na 6 adhabu yake ni faini isiyo chini ya Shilingi Milioni Tano (5,000,000/-) na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi (10,000,000/-) au kifungo kisichopungua miezi sita (6) na kisichozidi miezi 12 au adhabu zote kwa pamoja.

Kwa upande wa kosa namba 2,5 na 7 adhabu yake ni faini isiyo chini ya Shilingi Milioni Tatu (3,000,000/-) na isiyozidi Milioni Tano (5,000,000/-) au kifungo kisichopungua miezi sita (6) na kisichozidi miezi 12 au adhabu zote kwa pamoja.

Kifungu cha 57(2) kimeendelea kubainisha kuwa, Mtumishi wa Umma ambaye atakiuka masharti ya Sheria ya Serikali Mtandao, atastahili hatua za kinidhamu au kijinai kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma (sura 298) au sheria nyingine husika. Hatua hizi ni pamoja na kufukuzwa kazini, kuonywa, kupunguzwa cheo, karipio, kupunguzwa mshahara n.k

Sheria hii pia chini ya Kifungu cha 58(1) imetoa adhabu ya jumla kuwa, mtu ambaye atakiuka masharti yoyote ya Sheria hii ambapo adhabu maalum haijatolewa atakua ametenda kosa na atakapotiwa hatiani, basi atastahili kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili (2,000,000/-) na isiyozidi shilingi milioni ishrini (20,000,000/-) au kifungo cha muda usiopungua miezi sita na isiyozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja kifungo na faini.

Pamoja na adhabu tajwa, Sheria, chini ya kifungu cha 58(2) imeelekeza kuwa, kwa mtu ambaye atatiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria hii, basi mahakama pamoja na kutoa adhabu stahiki, inaweza kumuagiza mtu huyo kulipa kwa Mamlaka kiwango kinacholingana na gharama ya ukarabati wa uharibifu wowote uliosababiswa. Malipo hayo yatakua kama fidia ya uharibifu aliosababisha.

Ili kukuza matumizi ya TEHAMA serikalini, Mamlaka ya serikali Mtandao imeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha hilo, na ili kuepusha kukwamishwa kwa namna moja au nyingine sheria imeweka masharti ambayo kila mtumishi wa umma anapaswa kuyaepuka katika matumizi ya Serikali Mtandao, na kushindwa kufuata masharti hayo basi mtumishi huyo atapatiwa adhabu kwa mujibu wa sheria kama ilivotajwa hapo juu.




# e-GA YATOA ELIMU KWA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imetoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Kamati tendaji ya TEHAMA ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC).

Mafunzo hayo yaliyotolewa Oktoba 29, 2024 jijini Dodoma, yalilenga kuijengea uwezo kamati hiyo katika usimamizi na uendeshaji wa miradi na mifumo ya TEHAMA na namna kamati hiyo inavyowajibika katika ujenzi wa Serikali ya Kidijiti ndani ya taasisi.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC Bw.Ramadhani Kailima alisema kuwa, mafunzo hayo ni sehemu ya jithada za Tume hiyo katika kuhakikisha inatekeleza Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika uendeshaji wa miradi na mifumo ya TEHAMA ndani ya taasisi.

Aliongeza kwamba, mafunzo hayo pia ni sehemu ya maandalizi ya INEC kuelekea uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa mwaka 2025, ambapo TEHAMA ni nyenzo mojawapo kuhakikisha zoezi hilo linafanyika kwa ufanisi.

"Naipongeza sana Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kutujengea uwezo, wataalamu wake wametupitisha katika maeneo ya Sheria pamoja na usalama wa mifumo yetu pamoja na matumizi yake." alisema Bw.Kailima.

Naye Meneja wa Usimamizi wa Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao Bi. Sultana Seiff alisema, uwepo wa Kamati tendaji ya TEHAMA katika kila taasisi ni takwa la Kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Serikali Mtandao namba 10 ya mwaka 2019, kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 18 cha sheria hiyo.

"Kwa mujibu wa sheria, kamati hii ndiyo msimamizi mkuu wa utekelezaji wa masuala yote ya TEHAMA ndani ya taasisi, hivyo mafunzo tuliyotoa yamewajengea uwezo wajumbe ili kuhakikisha wanazingatia matakwa ya sheria, lakini pia kuhakikisha TEHAMA inatumika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji huduma kwa wananchi sambamba na kuhakikisha usalama wa mifumo na miundombinu ndani ya taasisi unazingatiwa" alifafanua Bi.Sultana.


Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Daftari na TEHAMA wa INEC Bw.Stanslaus Mwita alisema, mafunzo hayo yatawasaidia kutimiza majukumu yao kwa ufanisi na weledi katika kuratibu na kusimamia uchaguzi mkuu.
"Mafunzo haya kwetu ni muhimu sana,yamewaongezea uwezo wajumbe wa kamati kujua majukumu yao ndani ya taasisi ikiwemo kusimamia miradi na mifumo ya TEHAMA ikiwemo ile ya uchaguzi", alifafanua Mwita.
Utoaji wa elimu kuhusu Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, ni jukumu endelevu la Mamlaka ya Serikali Mtandao, katika kuhakikisha kamati hizo za taasisi zinajengewa uwezo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.



**"Wajumbe wa kamati ya Uongozi ya TEHAMA ya Tume Huru ya Uchaguzi wanashiriki mafunzo haya yanayohusu Sheria ya Serikali Mtandao nami nikiwa ni mwenyekiti wa kamati hii nimeshiriki mafunzo hayo kikamilifu ili sote tuwe na uelewa wa pamoja"**

**Bw.Ramadhani Kailima**
Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC

# KUTOKA KATIKA KITUO CHA UTAFITI, UBUNIFU NA UENDELEZAJI WA SERIKALI MTANDAO - eGOVRIDC




## MFUMO WA TSMS TOLEO LA PILI WABORESHWA KUIMARISHA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAFUNZO NA WARSHA

- Sasa ni Jumuishi
- Uratibu wa makongamano na Semina ni rahisi zaidi

Mfumo wa Uratibu, Usimamizi na Uendeshaji wa Mafunzo na Semina (Training and Seminar Management System - TSMS), toleo la pili 'version 2', umeboreshwa zaidi ili kuongeza ufanisi wa uendeshaji, usimamizi na uratibu wa mafunzo na semina, katika taasisi za umma.

Mfumo huu kwa sasa umeongezewa moduli sita kutoka moduli nane za awali na kufanya jumla ya moduli 14, zinazomuwezesha mtumiaji kutatua changamoto zote za uandaaji wa semina, kikao na mafunzo kidigiti tofauti na toleo la kwanza la mfumo huu. Akifafanua kuhusu maboresho hayo, Meneja wa Utafiti, Ubunifu na Mafunzo wa Serikali Mtandao (e-GA) Dkt. Jaha Mvulla, amebainishwa kuwa toleo la kwanza la mfumo wa TSMS (TSMS v1 ) lilikuwa mahsusi kwa matumizi ya e-GA pekee 'standalone' na haukuwa shirikishi 'shared system'.

Kutokana na uhitaji wa mfumo huu katika taasisi nyingine, e-GA ilianza kutoa msaada wa kiufundi katika taasisi hizo ili ziweze kunufaika kwa kuendesha semina kupitia mfumo huu, na hatimaye kufanya maboresho katika toleo la pili la mfumo, ili kila taasisi iweze kujihudumia.

"Toleo la kwanza la TSMS lilikuwa na moduli 8 tu zilizohusu matangazo ya vikao, semina na mikutano, usajili wa wajumbe wa mikutano na vikao, malipo, mahudhurio pamoja na kupata nyaraka muhimu za vikao, semina na mikutano" amefafanua Jaha.

Ameongeza kuwa, ingawa mfumo ulikuwa thabiti na wenye ufanisi kwa mahitaji ya awali, lakini ulikuwa na uwezo mdogo katika ufuatiliaji wa shughuli maalum kama ratiba, mafunzo, na mikutano ya mtandaoni jambo lililoipelekea e-GA kufanya maboresho zaidi katika mfumo ili kuendana na mahitaji.

Moduli sita zilizoongezeka ni moduli ya kuratibu hafla (Event Management), inayoruhusu usimamizi wa mipango ya matukio, Moduli ya Kuratibu Ratiba za Mafunzo (Training Plan Management) inayowezesha kuratibu mafunzo, usajili wa washiriki, ufuatiliaji wa matukio, na ripoti za baada ya tukio.



**Dkt. Jaha Mvulla**
Meneja wa Utafiti, Ubunifu na Mafunzo wa Serikali Mtandao(MRIT)

Moduli hii inamuwezesha mtumiaji kuhifadhi nyaraka muhimu kama muhutasari wa mikutano, mawasilisho, na nyaraka za mipango ya mafunzo na hivyo kupunguza utegemezi wa makaratasi, kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa haraka, na kuboresha usalama wa nyaraka.
Moduli nyingine ni moduli ya kupiga kura (Polling Module) inayowapa nafasi washiriki wa mafunzo au mkutano, kuweza kupiga kura na kufanya maamuzi yaliyopo mbele yao, kutoa maoni na kukusanya takwimu.

Vilevile, kuna moduli inayowezesha washiriki kufanya mtihani (Aptitude Test), moduli hii inaruhusu uundaji wa vipimo vya maarifa na uwezo wa washiriki wa mafunzo, muwezeshaji ana uwezo wa kutengeneza maswali na kupata majibu kutoka kwa washiriki wake ili kupima uelewa wao.

''Moduli nyingine liyoongezwa ni ile ya Mafunzo/Semina kwa njia ya Mtandao (Virtual Sessions), moduli hii imejumuisha mikutano ya mtandaoni, ikiruhusu mawasiliano ya moja kwa moja kwa njia ya video, sauti na mawasilishisho, hivyo hata mtu ambayo hayupo ukumbini mfumo utamuwezesha kutoa mada," amefafanua Dkt. Jaha.

Amebainisha kuwa, wadau mbalimbali wameshirikishwa katika upatikanji wa toleo hili la pili la mfumo wa TSMS kuanzia ngazi ya ukusanyaji wa mahitaji, usanifu, ujenzi na majaribo pamoja na kuzingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao.

Dkt. Jaha ametoa wito kwa taasisi za umma kutumia mfumo wa TSMS toleo la pili, ili kuokoa muda na gharama zinazotumika kusimamia mikutano na mafunzo sambamba na kuongeza ufanisi wa mafunzo hayo.

Mfumo wa TSMS V2 unapatikana kupitia www.tsms.gov.go.tz na umeunganishwa na mfumo wa malipo wa Serikali wa GePG ili kuwezesha mchakato wa malipo, kupata ripoti ya malipo kwa mafunzo, makongamano, mikutano na warsha zinazolipiwa
.
Pia, mfumo unawezesha kufanya malipo kwa njia ya VISA na Mastercard kwa watumiaji walioko nje ya nchi na umeunganishwa na Mfumo wa kuwezesha mifumo kubadilishana taarifa Serikalini wa GovESB, hivyo kuufanya mfumo huu kuweza kubadilisha taarifa na mfumo wowote wa Serikali inapohitajika.

# MATUKIO KATIKA PICHA

## MAONESHO - KONGAMANO LA 8 LA TEHAMA DAR ES SALAAM



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), akisikiliza taarifa ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na e-GA katika kukuza Serikali Mtandao nchini kutoka kwa Meneja Mawasiliano e-GA Bi Subira Kaswaga, wakati wa Maonesho ya kongamano la 8 la TEHAMA





Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry William Silaa (Mb.), akipata maelezo kutoka kwa Afisa Habari Mwandamizi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Queenter Mawinda, kuhusu Jitihada zinazofanywa na Mamlaka katika kuhakikisha ufanisi wa utendaji kazi wa Taasisi za Umma unaimarika kupitia TEHAMA

# MAONESHO - WIKI YA UBUNIFU WA HUDUMA ZA AFYA KIDIJITALI




Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama (MB), akisikiliza taarifa kuhusu jitihada zinazofanywa na e-GA kuwezesha huduma za Afya Kidijitali kutoka kwa Meneja wa Viwango na Miongozo wa e-GA Bi. Sultana Seiff, wakati wa Maonesho ya wiki ya Ubunifu wa Huduma za Afya kidijitali yaliofanyika Mlogazila Jijini Dar Es Salaam.




Mtumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Bw.Frank Alex(Kulia) akitoa maelezo ya huduma za Mamlaka kwa Mdau wa Serikali Mtandao aliyetembelea banda la Mamlaka ya Serikali Mtandao katika Maonesho wiki ya Ubunifu wa Huduma za Afya Kidijitali yaliofanyika Mlogazila Jijini Dar Es Salaam

# MAONESHO - WIKI YA UBUNIFU WA HUDUMA ZA AFYA KIDIJITALI




Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Bw. Mohammed Khamis Abdulla, akimkabidhi tuzo ya Shukrani ya Udhamini wa Wiki ya Ubunifu wa Huduma za Afya Meneja wa Usimamizi wa Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao wa e-GA Bi Sultana Seif.




Mdau wa Serikali Mtandao akipewa maelezo ya huduma za Mamlaka ya Serikali Mtandao kutoka kwa Mtumishi wa Mamlaka alipotembelea banda la Mamlaka ya Serikali Mtandao katika Maonesho ya wiki ya Ubunifu wa Huduma za Afya Kidijitali yaliyofanyika Mlogazila Jijini Dar Es Salaam

# MAONESHO - MKUTANO WA 9 WA MAMENEJA RASIMALIWATU NA UTAWALA BARANI AFRIKA




Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), akipata maelezo kutoka kwa Afisa Habari Mwandamizi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Queenter Mawinda, kuhusu Jitihada zinazofanywa na Mamlaka katika kuhakikisha ufanisi wa utendaji kazi wa Idara na Vitengo katika Taasisi za Umma unaimarika kupitia TEHAMA, alipotembelea banda la maonesho la e- GA Novemba 4, 2024 katika Mkutano wa 9 wa Mameneja Rasimali Watu na Utawala Barani Afrika uliofanyika Jijini Arusha.




Mdau wa Serikali Mtandao akipewa maelezo ya huduma za Mamlaka ya Serikali Mtandao kutoka kwa Mtumishi wa mamlaka alipotembelea banda la Mamlaka ya Serikali Mtandao (e- GA) katika Mkutano wa 9 wa Mameneja Rasimali Watu na Utawala Barani Afrika uliofanyika Jijini Arusha.

# MAONESHO - MAADHIMISHO YA WIKI YA VIJANA OCTOBA 2024



Mtumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Catherine Peter akitoa elimu kuhusu jitihada mbalimbali zinazofanywa na e-GA katika ujenzi wa Serikali kwa Mwananchi aliyetembelea banda la e-GA, katika Maonesho ya Kitaifa ya Wiki ya Vijana yaliyofanyika katika viwanja vya Furahisha jijini Mwanza.




Wananchi waliotembelea banda la Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), katika Maonesho ya Kitaifa ya Wiki ya Vijana yanayoendelea katika viwanja vya Furahisha jijini Mwanza, wakipewa elimu kuhusu jitihada mbalimbali zinazofanywa na e-GA katika ujenzi wa Serikali ya Kidijiti.

# UKAGUZI WA JENGO LA OFISI ZA e-GA DODOMA



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Boniface Simbachawene akitoa maelekezo kwa Mkandarasi wa Jengo la Mamlaka ya Serikali Mtandao wakati alipofanya Ukaguzi wa jengo hilo Mtumba Jijini Dodoma.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Boniface Simbachawene akifanya ukaguzi na kuangalia maendeleo ya ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Serikali Mtandao Jijini Dodoma.

# MAFUNZO - MFUMO WA HUDUMA KWA WATEJA



Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali mtandao Bw. Faraja Mpande (Kulia)akitoa mafunzo ya Mfumo wa Huduma kwa wateja kwa Maafisa TEHAMA kutoka taasisi mbalimbali za Umma.



Maafisa TEHAMA kutoka katika Taasisi za Umma wakifuatilia kwa makini mafunzo ya Mfumo wa Huduma kwa wateja yaliyotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao e-GA

# TUNAIMARISHA AFYA



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba (wa kwanza kushoto) akiongoza mazoezi ya watumishi wa e-GA ikiwa ni jitihada za kuimarisha afya za watumishi wa Mamlaka.





# BODI YA UHARIRI

## MWENYEKITI

Mhandisi Benedict B. Ndomba
Mkurugenzi Mkuu

## WAJUMBE

CPA (T) Salum Mussa
Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji

SACP Hamis Ali
Mkaguzi Mkuu wa Ndani

SACP Rafael Rutaihwa
Meneja wa Huduma za Sheria

Long'ida Oltetiai
Meneja wa Huduma kwa Wateja na Takwimu

## MHARIRI

Subira Kaswaga
Meneja Mawasiliano

## WAANDISHI

Catherine Peter | Afisa Habari Mwandamizi
Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

## WAPIGA PICHA

Mussa Enock |Afisa Habari
Ben Bago |Afisa Habari

## MSANIFU KURASA

Edger Msamba | Afisa TEHAMA